



**SWAHILI B – HIGHER LEVEL – PAPER 2**  
**SOUAHÉLI B – NIVEAU SUPÉRIEUR – ÉPREUVE 2**  
**SUAHILI B – NIVEL SUPERIOR – PRUEBA 2**

Friday 2 November 2007 (morning)  
Vendredi 2 novembre 2007 (matin)  
Viernes 2 de noviembre de 2007 (mañana)

1 h 30 m

---

**INSTRUCTIONS TO CANDIDATES**

- Do not turn over this examination paper until instructed to do so.
- Choose one task.

**INSTRUCTIONS DESTINÉES AUX CANDIDATS**

- Ne retournez pas cette épreuve avant d'y être autorisé(e).
- Choisissez une tâche.

**INSTRUCCIONES PARA LOS ALUMNOS**

- No dé la vuelta al examen hasta que se lo autoricen.
- Elija una tarea.

Andika maneno yasiyopungua 400 juu ya **mojawapo** ya haya yafuatayo.

1. Hivi majuzi ulipata fursa ya kuutazama mchezo wa kuigiza ulioigizwa na mojawapo wa kikundi maarufu cha uigizaji nchini mwako. Ulipendezwa mno na uigizaji wao. Mwandikie barua rafiki yako ukielezea yafuatayo: mchezo ulihusu nini, mambo yaliyokupendeza kwenye mchezo huu na kwa nini, na yale ambayo ulijifunza.
  2. Serikali yako imeanzisha kampeni kabambe za kuwashirikisha wanawake katika nyanja zote za maendeleo. Inadai kuwa “kuwahuzisha wanawake katika shughuli zote za kimaendeleo ni kulikuza taifa bora”. Huku ukitoa mifano, jadili nafasi ya wanawake katika: elimu, kazi na siasa katika jamii yako.
  3. Shule yako ingependa kuongeza idadi ya wanafunzi. Wewe ukiwa mwenyekiti wa klabu cha uandishi umeombwa kutoa mchango wako kusaidia kwenye kampeni hizi. Huku ukitoa mifano, andika makala ambayo yatatolewa kwenye mojawapo wa magazeti nchini mwako juu ya mambo manne ambayo unafikiri huifanya shule yako iwe bora.
  4. Hivi karibuni kumekuwa na malalamiko mengi katika jamii yako juu ya ongezeko la visa vya uhalifu. Wewe ukiwa mhariri wa gazeti la shule yenu umeombwa kumhoji mmojawapo wa wanafunzi wa zamani wa shule yako ambaye ni afisa mkuu wa polisi juu ya chanzo cha visa hivi, madhara and jinsi hali hii inaweza kurekebisha. Andika nakala ya mahojiano yenu.
  5. Unahoofishwa na ongezeko la ukosefu wa ajira na viwango vya umaskini nchini mwako. Andika barua kwa mhariri wa gazeti la *Taifa Leo*, ukipendekeza njia ambazo zinaweza kutumiwa kulisuluhisha tatizo hili.
  6. Shule yako ingependa kuweka kumbukumbu za historia yake kuhusu: chimbuko lake, ufanisi wake katika mitihani ya kitaifa, na maendeleo yake katika ujenzi wa shule. Wewe kama mwanachama wa klabu cha historia ambaye hivi majuzi umeshiriki kwenye mkutano wa kujadili uwezekano wa kuifanikisha shughuli hii umeombwa kumwandikia mkuu wa shule ripoti ya majadiliano yenu. Andika ripoti yako.
-